

DOYEN PUBLISHERS

KENYA JUNIOR SCHOOL EDUCATION ASSESSMENT

MTIHANI WA MUHULA WA 2 2025

GREDI YA 9 – KISWAHILI

(Kartasi ya 1 - Kiswahili Lugha)



Muda: Saa 1 dakika 40

JINA: _____

SHULE: _____

KITENGO: _____ TAREHE: _____

MAAGIZO KWA WATAHINIWA

- Andika jina lako, shule, kitengo na tarehe katika sehemu zilizo hapo juu.
- Karatasi hii ina maswali 50 ya uchaguzi wengi. Jibu MASWALI YOTE katika kijitabu hiki cha maswali.
- Majibu yote lazima yatolewe kulingana na miongozo ya maswali.
- Kwa kila swali kutoka 1 hadi 50, kuna majibu manne. Majibu haya yameandikwa A, B, C na D. Kila wakati, moja tu kati ya majibu manne ndio sahihi. Chagua jibu sahihi na uandike kwenye jedwali lililo chini.
- Fanya kazi zote za kujaribu kwenye karatasi ya maswali.

EST

JEDWALI LA MAJIBU

2023

1.	2.	3.	4.	5.	6.	7.	8.	9.	10.	11.	12.	13.	14.	15.	16.	17.	18.	19.	20.
21.	22.	23.	24.	25.	26.	27.	28.	29.	30.	31.	32.	33.	34.	35.	36.	37.	38.	39.	40.
41.	42.	43.	44.	45.	46.	47.	48.	49.	50.										

ALAMA ZA MTAHINIWA

Kutoka kwa 50	
---------------	--

Karatasi hii ina kurasa 5 zilizopigwa chapa. Watahiniwa wanapaswa kukagua karatasi hii ili kuhakikisha kuwa kurasa zote zimepigwa chapa kama ilivyosemwa na hakuna maswali yanayokosekana.

L'avenir commence ici

Page 1 of 5

DOYEN PUBLISHERS || 0780802443

Visit our website to access complete papers: www.doyenpublishers.com.

Soma kifungu kilichofuata kisha jibu swali la 1 hadi 7.

Katika kijiji cha Lindi, wakazi wameamua kushirikiana kuhakikisha mazingira yao ni safi na salama. Kila Jumamosi asubuhi, wanakutana pamoja kufanya shughuli za usafi kama kufyeka nyasi, kuokota taka na kusafisha mitaro. Mwenyekiti wa kijiji, Bwana Juma, anasisitiza kuwa mazingira safi huchangia afya bora kwa jamii nzima. Watoto nao hufundishwa umuhimu wa kutupa taka kwenye mapipa maalum na kutunza mazingira yao.

Mbali na shughuli za kila wiki, viongozi wa kijiji wameanzisha kampeni ya kupanda miti ili kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. Wanakijiji wanahimizwa kupanda angalau mti mmoja kila mwezi. Kupitia juhudi hizi, kijiji cha Lindi sasa kinajulikana kwa usafi wake na mazingira ya kijani kibichi. Wageni wengi wanaotembelea kijiji hicho hupongeza juhudi hizo na kujifunza kutoka kwao.

- | | |
|--|---|
| 1. Ni lini wanakijiji wa Lindi hukutana kwa usafi?
A. Kila Jumapili
B. Kila siku
C. Kila Jumamosi
D. Kila mwezi | 5. Kampeni ya kupanda miti inalenga nini?
A. Kukusanya taka
B. Kupunguza joto
C. Kurekebisha mitaro
D. Kuzuia mvua |
| 2. Nani anasisitiza umuhimu wa mazingira safi?
A. Watoto wa kijiji
B. Wageni wa kijiji
C. Mwenyekiti wa kijiji
D. Walimu | 6. Kijiji cha Lindi kinajulikana kwa nini sasa?
A. Ukame na joto
B. Magonjwa mengi
C. Usafi na mazingira ya kijani
D. Uvivu wa wakazi wake |
| 3. Watoto hufundishwa nini kuhusu mazingira?
A. Kupanda miti tu
B. Kukusanya taka nyumbani
C. Kutupa taka ovyo
D. Kutupa taka kwenye mapipa maalum | 7. Wageni hujifunza nini wanapotembelea Lindi?
A. Jinsi ya kuvua samaki
B. Mbinu za biashara
C. Jinsi ya kutunza mazingira
D. Jinsi ya kulima |
| 4. Kwa nini wanakijiji wanapanda miti?
A. Kwa mapambo tu
B. Kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi
C. Kwa ajili ya kuni
D. Kufanya kivuli | |

Soma kifungu kilichofuata kisha jibu swali la 8 hadi 13.

Katika mji wa Makutano, ajali nyingi ziliripotiwa kwa sababu ya watu kutofuata sheria za barabarani. Madereva walikuwa wakiendesha kwa kasi kupita kiasi, wakati waendao kwa miguu walikuwa wakivuka barabara pasipo kutumia vivuko maalum. Kutokana na hali hii, serikali ya kaunti ilianzisha kampeni ya usalama barabarani ili kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kufuata sheria.

Shule mbalimbali zilihusishwa katika kampeni hiyo, ambapo wanafunzi walifundishwa jinsi ya kutumia alama za barabarani, kupisha magari, na kuvuka barabara kwa usalama. Aidha, askari wa trafiki waliongezwa barabarani ili kusaidia kudhibiti mienendo ya madereva. Hali ya usalama imeimarika, na ajali zimepungua kwa kiasi kikubwa.

- | | |
|--|--|
| 8. Ni nini kilisababisha ajali nyingi Makutano?
A. Upungufu wa magari
B. Matuta ya barabarani
C. Watu kutofuata sheria za barabarani
D. Kuongezeka kwa watalii | 9. Ni nani alianzisha kampeni ya usalama barabarani?
A. Shule binafsi
B. Serikali ya kaunti
C. Madereva wa mabasi
D. Wananchi wa kawaida |
|--|--|

10. Kampeni ya usalama ilihusisha nani?

- A. Wakulima pekee
- B. Wafanyabiashara tu
- C. Shule mbalimbali
- D. Madaktari

11. Askari wa trafiki waliongezwa kwa lengo gani?

- A. Kulinda benki
- B. Kufundisha madereva kuendesha
- C. Kudhibiti mienendo ya madereva
- D. Kupiga picha barabarani

12. Vivuko maalum hutumika kwa kazi gani?

- A. Kupita magari makubwa
- B. Kupumzika njiani
- C. Kuvuka barabara kwa usalama
- D. Kuonyesha matangazo

13. Nini kilitokea baada ya kampeni kuanzishwa?

- A. Ajali ziliongezeka
- B. Shule zilifungwa
- C. Ajali zilipungua
- D. Barabara zilifungwa

Soma kifungu kilichofuata kisha jibu swali la 14 hadi 20.

Jamii nyingi nchini zinakumbwa na changamoto kama vile ukosefu wa ajira, matumizi ya dawa za kulevya, na migogoro ya kifamilia. Katika mtaa wa Mlimani, vijana wengi hawana kazi, jambo ambalo linawasukuma kujiingiza katika uhalifu na matumizi ya mihadarati. Hali hii imesababisha hofu miongoni mwa wakazi, huku wazazi wakihofia mustakabali wa watoto wao.

Mashirika yasiyo ya kiserikali yameanza kuingilia kati kwa kutoa mafunzo ya ufundi kwa vijana kama useremala, ushonaji na upishi. Lengo ni kuwapa stadi zitakazowasaidia kujitegemea badala ya kutegemea ajira rasmi. Pia, vikundi vya ushauri nasaha vimeanzishwa ili kusaidia familia zilizoathirika kisaikolojia. Hii imeleta matumaini mapya katika jamii.

14. Ni changamoto zipi zinazoikumba jamii?

- A. Barabara mbaya tu
- B. Uharibifu wa mazingira
- C. Ukosefu wa ajira na dawa za kulevya
- D. Uhaba wa shule

15. Neno '*changamoto*' lina maana sawa na neno gani hapa chini?

- A. Mafanikio
- B. Suluhisho
- C. Tatizo
- D. Faraja

16. Kwa nini vijana wa Mlimani hujiingiza kwenye uhalifu?

- A. Kwa sababu ya elimu duni
- B. Kwa sababu ya ushawishi wa familia
- C. Kwa sababu hawana kazi
- D. Kwa sababu ya muziki

17. Mashirika yasiyo ya kiserikali yanasaidia vipi?

- A. Kwa kutoa msaada wa chakula
- B. Kwa kutoa mafunzo ya ufundi
- C. Kwa kujenga nyumba
- D. Kwa kuwapa kazi za serikali

18. Vikundi vya ushauri nasaha:

- A. Huvinjari mtandaoni
- B. Hutoa chakula
- C. Husaidia familia kisaikolojia
- D. Hufundisha sheria

19. Lengo la mafunzo hayo ni lipi?

- A. Kupunguza kodi
- B. Kuwafanya vijana wafungwe
- C. Kuwasaidia kujitegemea
- D. Kuwafanya wafanye kazi ngumu

20. Matokeo ya juhudi hizi ni yapi?

- A. Jamii imevurugika zaidi
- B. Matumaini mapya yamezaliwa
- C. Vijana wamehamia miji mikuu
- D. Elimu imeporomoka

Soma kifungu kilichofuata kisha jibu swali la 21 hadi 25.

Familia ya Bi. Amina ilipatwa na huzuni kubwa baada ya mtoto wao wa miezi mitatu kufariki katika hospitali ya wilaya. Kwa mujibu wa mama huyo, walifika hospitalini saa mbili asubuhi lakini hawakuhudumiwa kwa haraka kutokana na ukosefu wa wahudumu wa afya. Mtoto alikuwa na homa kali na alihitaji matibabu ya dharura. Licha ya kulia na kuomba msaada, walichelewa kuhudumiwa na mtoto alifariki kabla ya saa sita mchana.

Baada ya tukio hilo, wakaazi wa mtaa huo waliandamana wakitaka haki itendeke na huduma za afya ziborewe. Serikali ya kaunti iliahidi kuchunguza tukio hilo na kuongeza wahudumu wa afya hospitalini. Pia, hospitali hiyo ilipokea vifaa vipya vya matibabu na mafunzo kwa wahudumu wake. Hali hiyo ilizua mjadala mpana kuhusu hali ya huduma za afya nchini na haja ya kuweka maisha ya watu mbele ya yote.

- | | |
|--|--|
| 21. Kulingana na mama, kwa nini hawakuhudumiwa haraka?
A. Walifika hospitali usiku
B. Kulikuwa na mgomo wa wauguzi
C. Hakukuwa na wahudumu wa afya wa kutosha
D. Walichelewa kuingia | 24. Serikali ya kaunti ilichukua hatua gani?
A. Ilifunga hospitali
B. Ilipandisha bei ya matibabu
C. Ilihidi kuchunguza na kuongeza wahudumu
D. Iliongeza kodi |
| 22. Mtoto alifariki saa ngapi?
A. Kabla ya saa sita mchana
B. Saa mbili asubuhi
C. Saa kumi jioni
D. Usiku wa manane | 25. Kinyume cha neno 'maisha' ni?
A. Mauti
B. Magonjwa
C. Maumivu
D. Mzazi |
| 23. Wananchi walifanya nini baada ya tukio hilo?
A. Walikaa kimya
B. Walihamia hospitali nyingine
C. Waliandamana kutafuta haki
D. Walizomea serikali | |

Soma kifungu kifuatacho kisha chagua jibu sahihi kwa kila nafasi.

Uhuru ni neno 26 watu wengi hilitumia 27 sana. Siku hizi jambo 28 likitokea watu 29 kwema. Kusema uhuru 30 au haki 31 si vyema. Subira huvuta 32, tukiwa watu 33 subira. Pia tutayatatua matatizo 34 bila kuandamana 35 barabara bila mtu kusikia kilio chetu.

- | | A | B | C | D |
|-----|----------|----------|------------|------------|
| 26. | ambayo | ambalo | ambazo | ambacho |
| 27. | vibaya | mbaya | kwa | kilio |
| 28. | ndogo | dogo | kidogo | kindogo |
| 29. | hukimbia | kimbilia | hukimbilia | wanakimbia |
| 30. | yetu | zetu | wetu | wet |
| 31. | yetu | zetu | wenye | zet |
| 32. | heri | njeri | zetu | wenye |
| 33. | wenye | wana | wasio | walio |
| 34. | yetu | zetu | wenye | yao |
| 35. | kwenye | kwa | heri | malalamiko |

L'avenir commence ici

Page 4 of 5

DOYEN PUBLISHERS || 0780802443

Visit our website to access complete papers: www.doyenpublishers.com.